# Yatupasa Kumshukuru Mungu

Peter Makolo
Jan. 2013
Kumbukumbu ya siku yangu ya kuzaliwa
Goteborg, Sweden






2. Ninajua Mungu wetu ni mwema sana
Nashuhudia waziwazi ni mwema sana

Katutunza mpaka sasa ona tunavyopendeza
Ametupa familia nzuri na za kupendeza

Hatuna cha kumlipa (Bwana wetu)
Kwa upendo wake,

{Yatupasa kumshukuru Mungu
Siku za maisha yetu yote} x2

3. Ninajua Mungu wetu ni mwema sana
Nashuhudia waziwazi ni mwema sana

Anatupa mahitaji ya muhimu siku zote
Yupo nasi tutokapo yupo nasi turudipo

Hatuna cha kumlipa (Bwana wetu)
Kwa upendo wake,

{Yatupasa kumshukuru Mungu
Siku za maisha yetu yote} x2

4. Ninajua Mungu wetu ni mwema sana
Nashuhudia waziwazi ni mwema sana

Ametupa maarifa ya kupambanua mambo
Katujaza na Hekima tuweze kuelewana

Hatuna cha kumlipa (Bwana wetu)
Kwa upendo wake,

{Yatupasa kumshukuru Mungu
Siku za maisha yetu yote} x2

5. Ninajua Mungu wetu ni mwema sana
Nashudia waziwazi ni mwema sana

Tumrudishie nini kwa Upendo wake kwetu
Kinacholingana na fadhili zake kwetu sisi

Hatuna cha kumlipa (Bwana wetu)
Kwa upendo wake,

{Yatupasa kumshukuru Mungu
Siku za maisha yetu yote} x2